**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JMT KATIKA KUMBUKIZI YA BABA WA TAIFA MWL. JULIUS NYERERE, KILELE CHA MBIO ZA MWENGE WA UHURU NA WIKI YA VIJANA KITAIFA, 2025

**MBEYA**
**14 OKTOBA, 2025**

- ***Mhe. Kassim Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa JMT;***
- ***Mhe. Hamza Hassan Juma, WN, Ofisi ya Makamu wa Pili, Zanzibar k.n.y. Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar;***
- ***Mhe. Tulia Akson; Spika, Bunge la JMT, & Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani;***
- ***Mhe. Zubeir Ali Maulid, Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar;***
- ***Mwakilishi wa Jaji Mkuu;***
- ***Mhe. John Mongella, Naibu Katibu Mkuu, CCM Tanzania Bara;***
- ***Mhe. William Lukuvi, WN, OWM – Sera, Bunge na Uratibu;***
- ***Mhe. Ridhiwani Kikwete, WN, OWM- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;***
- ***Mhe. Tabia Mwita Maulid, Waziri - Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo SMZ;***
- ***Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri;***
- ***Mhe. Beno Malisa, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, na Wahe. Wakuu wa Wilaya wote mliopo;***
- ***Wahe. Wananchi wa Mkoa wa Mbeya na Mikoa Jirani***
- ***Naheshimu Itifaki yote kama ilivyokwisha kutambulishwa.***

**JMT.....Baba wa Taifa Oyee...Mwenge wa Uhuru Oyee...Vijana Oyee...!**

## 1. Salamu

Napenda kuanza hotuba yangu kwa kumshukuru Mungu, aliyetuwezesha kujumuika hapa Jijini Mbeya kwa ajili ya matukio matatu kwa pamoja, yaani: kumbukizi ya miaka 26 ya kifo cha Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere; kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2025; na Wiki ya Vijana Kitaifa. Namshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa JMT kwa kunipa heshima ya kumwakilisha kwenye maadhimisho haya. Aidha, namshukuru Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa JMT, Viongozi na watendaji wote wa OWM - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (SMZ) kwa uratibu mzuri wa maadhimisho haya.

Vilevile, nampongeza na kumshukuru Mhe. Beno Malisa, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, pamoja na viongozi, watendaji na wananchi wote wa mkoa huu, kwanza kwa kuridhia kuwa wenyeji wa maadhimisho haya, na pili kwa ukarimu wenu kwa wageni wote waliokuja kushiriki tukio hili kubwa. Nawapongeza sana kwa maandalizi mazuri na maadhimisho haya ya viwango vya juu. **Hongereni sana.**

**Ndugu Wananchi,** kwa namna ya pekee nawapongeza na kuwashukuru vijana wetu waliokimbiza Mwenge wa Uhuru mwaka huu 2025, kwa kutekeleza jukumu hili kwa uzalendo, ustadi na ari kubwa. Hakika mmetekeleza jukumu hili kwa weledi, mkiongozwa na kaulimbiu inayowahimiza wananchi kushiriki katika uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu, na pia kuwahamasisha wananchi kufanya kazi kwa bidii, kuwajibika, kudumisha uzalendo, kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya na ufisadi, pamoja na kuhamasisha lishe bora na maendeleo ya jamii. Narudia tena kuwashukuru na kuwapongeza kwa kuwa mmelitendea haki Taifa lenu. **Hongereni na asanteni sana.**

## 2. Kumbukumbu ya miaka 26 ya kifo cha Baba wa Taifa

**Ndugu Wananchi,** tarehe 14 Oktoba 1999 ni siku ambayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliaga dunia. Hivyo, ni siku ambayo kila mwaka tunafanya kumbukizi ya maisha na mchango wake katika ujenzi wa Taifa letu, kisiasa, kijamii na kiuchumi. Tunapofanya kumbukizi ya Mwalimu Nyerere, tunasherehekea maisha yake ambayo aliyatoa katika kulitumikia Taifa letu, ambalo alilipenda sana. Baba wa Taifa alitoa mchango mkubwa sana katika kupigania uhuru wa nchi yetu, ambapo aliwaongoza viongozi wenzake kudai uhuru kutoka kwa Wakoloni na kufanikisha kupatikana kwa uhuru kamili mnamo tarehe 9 Desemba, 1961. Aidha, Baba wa Taifa kwa kushirikiana na Sheikh Abeid Amani Karume, waliwezesha kuunganishwa kwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na kuunda Taifa moja huru la Tanzania. Baba wa Taifa anakumbukwa pia kwa jitihada zake za kujenga umoja wa kitaifa kwa kuunganisha watu wa makabila zaidi ya 120 na jamii mbalimbali. Katika azma hiyo, alikuza matumizi ya lugha ya kiswahili kama nyenzo ya kuwaleta wananchi pamoja, kupinga aina zote za migawanyiko, na hivyo kuunda umoja imara wa kitaifa.

Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere pia alitoa mchango mkubwa sana kwa Taifa letu kwa kubuni na kutekeleza mpango wa wananchi wote kujua kusoma na kuandika. Alitekeleza sera ya elimu-msingi kwa wote bila malipo (free universal primary education) kwa kuwa aliamini kuwa elimu ndiyo silaha pekee ya kujikomboa na kujiletea maendeleo. Mwalimu katika uongozi wake alisisitiza usawa, haki za binadamu na utawala wa sheria unaotokana na matakwa ya watu walio wengi. Aidha, aling'atuka na kufanikiwa kukabidhi madaraka kwa hiyari kwa kiongozi mwingine, jambo ambalo lilimpatia heshima kubwa kote duniani. Alikuwa Mwanamajumui halisi aliyepigania umoja wa bara letu la Afrika (Pan - Africanist) na katika hilo alikuwa mstari wa mbele kusaidia harakati za ukombozi katika nchi mbalimbali kusini mwa Afrika.

Ili kuendelea kuenzi maisha na mchango mkubwa wa Baba wa Taifa, Watanzania wote tunatakiwa kusimamia misingi mikuu aliyotuachia Mwl. Julius Nyerere. Naomba nisisitize mambo manne tu kwa kifupi: Kwanza , kulinda uhuru wa Taifa letu pamoja na kudumisha umoja na amani na kusimamia haki miongoni mwa jamii yetu. Tusipofanya hayo kwa dhati, kuna hatari Taifa letu kusambaratika. Pili, kujenga na kuimarisha maadili mema katika jamii yetu, hususan miongoni mwa vijana wetu ambao ndiyo Taifa la sasa na la kesho. Ni lazima kukemea mmomonyoko wa maadili, ikiwemo rushwa na ufisadi, ambavyo Baba wa Taifa alivichukia sana na kuvipiga vita kwa vitendo. Tatu, ni kuwajibika kwa kila mwananchi kufanya kazi kwa bidii ili kuboresha maisha na kuinua vipato vyetu na hivyo kuchangia katika ujenzi wa Taifa. Nawahimiza vijana kuchangamkia fursa zilizopo na zinazochipuka katika sekta mbalimbali kama kilimo-biashara, ujasiriamali, TEHAMA, huduma (services) na pia michezo, sanaa na utamaduni.Kila mmoja wetu hana budi atambue kuwa anao wajibu katika kuijenga nchi yetu ya Tanzania. Tanzania itajengwa na Watanzania wenyewe. Nne, ni uhifadhi na utunzaji wa mazingira, hususan kulinda vyanzo vya maji, upandaji wa miti na kufanya usafi wa mazingira, mambo ambayo Baba wa Taifa alikuwa mfano bora wa kuigwa.

3. **Falsafa ya Mwenge wa Uhuru**

**Ndugu Wananchi,** leo pia tunahitimisha Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2025, ambao umekimbizwa katika mikoa na wilaya zote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu tarehe 2 Aprili, 2025 ulipowashwa rasmi Kibaha, Mkoani Pwani. Mwenge wa uhuru ulipoasisiwa ulilenga kuidhihirishia dunia na kuonesha mfano kwa Mataifa yaliyokuwa bado chini ya udhalimu wa kikoloni, maana ya Taifa huru na uwezo wetu wa kujitawala pasipo kuingiliwa na mtu mtu yeyote. Maono haya ya Mwalimu Nyerere yalikuwa sahihi, hususan kwa Taifa ambalo lilikuwa ndiyo kwanza limejinasua kutoka katika makucha ya wakoloni, aliposema ***"Sisi tumekwisha kuwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu, ulete matumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo mahali ambapo pana chuki na heshima ambapo pamejaa dharau."*** Falsafa hii imekuwa dira ya Mbio hizi kwa miaka yote, ikiendeleza dhamira ya kuhamasisha uzalendo na ujasiri wa kupambana na maovu katika jamii na kuleta amani, upendo, maendeleo na mshikamano katika Taifa letu na Mataifa mengine. Kupitia falsafa hii, nchi imefanikiwa katika mambo mengi ikiwemo kuondoa ubaguzi, ukabila, na kujenga umoja wa kitaifa; kuimarisha utawala bora; kupinga dhuluma, dharau, chuki na kupambana na ufisadi/rushwa. Kwa mantiki hiyo, Serikali itaendelea kuenzi falsafa hii kwa maendeleo ya Taifa letu.

**Ndugu Wananchi,** Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu zilijielekeza mahsusi kuhimiza ushiriki wa wananchi katika Uchaguzi Mkuu mwaka huu kwa kaulimbiu isemayo: ***"Jitokeze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu."*** Kwa kuzingatia matakwa ya kikatiba na kisheria, uchaguzi Mkuu umepangwa kufanyika tarehe 29 Oktoba 2025 chini ya usimamizi wa Tume Huru ya Taifa ya uchaguzi (INEC) na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC). Kupitia hadhara hii, nami naomba niongeze sauti yangu kuwaomba Watanzania wote waliojiandikisha kupiga kura kushiriki katika kampeni za uchaguzi zinazoendelea ili kusikiliza sera za vyama mbalimbali, na kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi ili kuwachagua viongozi watakaotuongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Hapa, napenda kuwakumbusha wananchi wenzangu kuzingatia wosia wa Baba wa Taifa kuhusu kuchagua viongozi waadilifu, watakaokidhi matarajio ya Watanzania na kuleta mabadiliko.

4. **Wiki ya Vijana Kitaifa**

**Ndugu Wananchi,** takwimu zinaonesha kuwa takriban 77.3% ya Watanzania wapo chini ya umri wa miaka 35. Hakika kaulimbiu ya Wiki ya Vijana Kitaifa mwaka huu inayosema "Nguvukazi ya Vijana kwa Maendeleo Endelevu" inaakisi ukweli huu. Kutokana na ukubwa na umuhimu wa Kundi hili, Serikali imeendelea kuadhimisha Wiki ya Vijana kitaifa ili kutambua mchango wao katika ujenzi wa Taifa. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza vijana wote nchini kwa mchango wenu mkubwa katika ujenzi wa Taifa na kwa ushiriki mzuri katika Wiki yenu. Kupitia maonesho ya Wiki ya Vijana hapa Mbeya, vijana wameonesha uwezo mkubwa katika ujasiriamali na matumizi ya teknolojia katika sekta mbalimbali za

maendeleo. Nawahimiza vijana muendelee kutumia ubunifu, maarifa na nguvu zenu vizuri zaidi na Serikali inawaamini na itawaunga mkono. Kwa kuzingatia hilo Serikali imeendelea kuwekeza kwenye elimu, ujuzi, teknolojia, ubunifu, michezo na utamaduni ili kuwajengea vijana uwezo wa kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2025 – 2030) imeweka lengo la kuanzisha vituo vya uwezeshaji vijana kiuchumi katika mikoa, pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana zipatazo milioni 8.5 ifikapo 2030. Ninapenda kuzikumbusha Wizara zetu mbili zenye dhamana ya Vijana kuratibu vema utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana na kuhakikisha sekta zote zinatekeleza ajenda ya kukuza ushiriki wa Vijana katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

## 5. Kitabu cha historia ya miaka 60 ya Mbio za Mwenge wa Uhuru (1964 – 2024)

**Ndugu Wananchi,** muda mfupi uliopita nimepokea maelezo kuhusu Kitabu cha Historia ya Miaka sitini (60) ya Mbio za Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo hivi punde nitapata fursa ya kukizindua. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu muhimu za Kihistoria, hususan Chimbuko, Maendeleo na Mchango wa Mbio za Mwenge wa Uhuru katika kujenga Mshikamano wa Kitaifa, Uzalendo na kuhamasisha maendeleo. Kitabu hiki pia kinaelezea umuhimu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kama alama ya mshikamano wa Watanzania wote bila kujali tofauti zetu za dini, kabila au itikadi. Namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (SMZ) kwa kuona umuhimu wa kutunza historia ya Taifa letu kupitia kitabu hiki cha miaka 60 ya Mbio za Mwenge wa Uhuru. Kitabu hiki ni urithi na rejea muhimu kwani kinatufundisha na kutukumbusha kuhusu haki, usawa, amani, umoja na mshikamano wa kitaifa tulionao, ambao msingi wake ulijengwa na waasisi wetu kupitia Mwenge wa Uhuru na falsafa yake. Kutokana na hazina iliyomo katika kitabu hiki, nashauri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iangalie uwezekano wa kukitumia kama nyenzo ya kufundishia Watoto na Vijana wetu shuleni na vyuoni.

## 6. Hitimisho

**Ndugu wananchi,** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwakumbusha na kuwasihi kuwa tunao wajibu wa kukuza uzalendo, kufanya kazi kwa bidii, kuheshimu sheria za nchi, na kutunza mazingira ili kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo. Vilevile, kuendelea kuthamini na kuiweka hai falsafa ya Mwenge wa Uhuru kama Tunu ya Taifa inayoakisi maono ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na waasisi wenzake. Aidha, ninawasihi nyote kujitokeza kwa wingi kupiga kura tarehe 29 Oktoba, 2025, ili kuchagua viongozi waadilifu, wazalendo na wenye maono ya kuipeleka Tanzania mbele. Nawasihi sana wananchi wote na hususan vijana kuhakikisha tunadumisha amani na utulivu wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza**